

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA HAKI ZA BINADAMU
NA UTAWALA BORA



Simu: +255734047775
Barua pepe: info@chragg.go.tz
Tovuti: www.chragg.go.tz

Kilimani,
Mtaa wa Nyerere,
S.L.P. 1049,
DODOMA,

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Tamko la THBUB Wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, 2022

Kila ifikapo Machi 8 ya kila mwaka, mataifa huwa yanaadhimisha Siku ya Mwanamke Duniani. Lengo la siku hii ni kutambua utu, nafasi na mchango wa mwanamke katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Umoja wa Mataifa uliridhia na kuanza kuadhimisha rasmi Siku ya Wanawake Duniani, Machi 8, 1975 kwa lengo la kuikumbusha Dunia juu ya usawa wa kijinsia na haki za wanawake.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inatambua na kuthamini jitihada mbalimbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kumwinua na kumpa heshima mwanamke ikiwemo kuongeza nafasi za ushiriki katika ngazi za maamuzi; kuweka mifumo ya kuwawezesha wanawake kiuchumi; kuimarisha miundombinu inayorahisisha upatikanaji wa huduma za afya kwa mama na mtoto; kuwarejesha watoto wa kike waliopata ujauzito katika mifumo ya elimu; na kuanzishwa kwa kituo Jumuishi cha Huduma za Kimahakama (One Stop Judicial Centre) iliyopo Wilayani Temeke kinachoshughulikia mashauri yanayohusu mirathi, ndoa na talaka pamoja na Mahakama Maalum inayoshughulikia mashauri ya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia kwa upande wa Zanzibar.

Kipekee, THBUB inampongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar kwa kuendeleza na kusimamia haki za binadamu, ikiwemo haki za wanawake na misingi ya utawala bora nchini.

Pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Serikali na Wadau mbalimbali katika kuhakikisha haki za wanawake zinalindwa na kuendelezwa, bado kuna changamoto ikiwemo udhalilishaji na ukatili dhidi ya wanawake; uwepo wa wa vifungu vya sheria vinavyohitaji marekebisho hususan katika masuala ya mirathi na ndoa na kuendelea kuwepo kwa mila potofu dhidi ya wanawake.

THBUB inaahidi kuendelea kutekeleza majukumu yake ya kulinda, kukuza, na kuhifadhi haki za binadamu na misingi ya utawala bora ili kuhakikisha kizazi cha haki na usawa kwa maendeleo endelevu nchini. Pamoja na hayo, THBUB inapendekeza yafuatayo:

1. Serikali

- lendelee kusimamia usawa na kutoa fursa kwa wanawake kushiriki kwenye ngazi za maamuzi, shughuli za kiuchumi na kijamii.
- Ifanye marekebisho ya sheria ili kuhakikisha usawa katika jamii.

2. Wadau

- Waongeze juhudi za kuelimisha jamii ili iachane na mila potofu.
- Wasiyafumbie macho matukio yenye kushusha utu wa mwanamke ili kujenga kizazi chenye kuheshimu usawa.

THBUB inawatakia maadhimisho mema ya siku ya Wanawake Duniani!

“Kizazi cha haki na usawa kwa maendeleo endelevu.”

Imetolewa na:

Mathew P.M. Mwaimu (Jaji Mstaafu)

MWENYEKITI

Machi 8, 2022